



# 2- SWALA NA TWAHARA

## Twahara na Aina za Maji

### 1-Utwahara kutokana na hadathi (hali ya kutokuwa na udhu na kuwa na janaba)

Hadathi ni kile kinachotokea katika mwili kikamzuia Mwislamu kufanya ibada ambazo zinahitaji utwahara, kama kuswali, kutufu kwenye Alkaba na zinginezo. Na inagawanyika vigawanyo viwili:
Hadathi Ndogo
Ni ile inayopasisha kutawadha kama vile kukojoa, kwenda haja kubwa na vitanguaji udhu vingine. Kujitwahirisha kwake kunakuwa kwa kutawadha. Mwenyezi Mungu U Anasema: {Enyi

mlioamini! Mkiinuka kutaka kuswali, osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpanguse vichwa vyenu na mwoshe miguu yenu mpaka vifundoni} (5: 6)
Hadathi Kubwa
Hiyo ni ile inayopasisha kuoga kama vile janaba, hedhi na vinginevyo. Na kujitwahirisha nayo inakuwa kwa kuoga. Mwenyezi Mungu U Anasema i: {Na mkiwa na janaba, jitwahirisheni} (5: 6)

### 2. Kujitwahirisha na Najisi:

Nao ni kuiyondoa najisi mwilini na nguoni na sehemu ya kufanya ibada, Na kuondoa najisi ni lazima kwa neno la Mwenyezi Mungu U: {Na nguo zako zitwahirishe} (74: 4)
na neno lake Mtume (s.a.w) [Mmoja wenu akija msikitini na atazame, akiona uchafu au kitu cha kuudhi kwenye viatu vyake basi na avipanguse kisha aswali navyo]

# Kutawadha

Udhu ni Kutumia maji kwenye viungo maalumu kwa nia ya kujitwahirisha

## Hukumu ya kutawadha

Kutawadha: ima ni lazima na ima inapendekezwa:

### a. Ni lazima kutawadha kwa mambo matatu

### 1. Kuswali

Mwenyezi Mungu U Anasema: {Enyi Mlioamini! Mnapo simama kwa ajili ya swala basi osheni nyuso zenu, na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa vyenu, na osheni miguu yenu mpaka vifundoni} [5: 6]

### 2. Kutufu Alkaba:

Kwa kauli yake Mtume ﷺ kumwambia mwanamke aliye katika hedhi: (Usitufu mpaka utwahirike) [ Imepokewa na Bukhari.].

### 3. Kushika Msahafu:

Kwa neno lake Mwenyezi Mungu U: {Hawaigusi isipokuwa wale waliotwahiriwa} [56: 79]

### b. Kutawadha kunasuniwa katika mambo mengine yasiyokuwa hayo

Kwa neno lake Mtume ﷺ aliposema: (Hajilazimishi na udhu isipokuwa mwenye Imani) [ Imepokewa na Ahmad].

Na kunapendekezwa zaidi kutawadha wakati wa kujadidisha udhu kwa kila Swala, kutawadha kwa kumtaja Mwenyezi Mungu na kuomba, wakati wa kusoma Qur'ani, kabla ya kulala, kabla ya kuoga, na kutokana na kumbeba maiti na baada ya kila tukio la kutangua udhu, hata kama hataki kuswali

## Namna ya kutawadha

## NAMNA YA KUTAWADHA HATUA KWA HATUA.

# Hatua ya 1 – weka nia ya kutia udhu.

Hamna matamshi au dua maalum ya udhu Bali nia ni makusudio ya kujitwahirisha.Nia au makusudio Mahali pake ni moyoni.

# Hatua ya 2 – Sema Bismillah بسم الله

# Hatua ya 3 – Kuosha vitanga viwili vya mkono.(mara tatu)

Anza na  upande wa kulia kwanza kwa hatua zako zote na hii ni kwa kila jambo. Osha hadi baina au katikati ya vidole.



# Hatua ya  4 – Kusukutua (mara tatu)



# Hatua ya 5 – Istinshaaq: (mara tatu)

Hapa ni kuweka maji ndani ya pua na kusafisha



# Hatua ya 6 – Kuosha uso (mara tatu)

Kuosha uso (mara tatu) pamoja na kupitisha maji ndani ya ndevu. Na mpaka wa uso kiurefu ni kuanzia mameleo ya nywele za kichwa mpaka chini ya kidevu, na kiupana ni kuanzia sikio mpaka sikio.



# Hatua ya 7 – Kuosha mkono kuanzia ncha za vidole mpaka vifundoni (mara tatu)

Kuosha mkono wa kulia kuanzia ncha za vidole mpaka kifundoni (mara tatu), kisha mkono wa kushoto kama hivyo.



# Hatua ya 8 – pangusa kichwa mara moja.

Kupangusa kichwa kwa  kupukusa mwanzo wa kichwa mpaka kwenye kishogo chake kisha kuurudisha mwanzo wake mara nyingine (mara moja).



# Hatua ya 9 – Kupangusa masikio mawili (mara moja)

kupangusa katikati mwa sikio kwa kidole cha shahada, na inje yake kwa kidole cha gumba (mara moja)



## Hatua ya 10 – Kuosha miguu hadi kwenye vifundo (mara tatu)

Kuosha mguu wa kulia hadi kwenye vifundo (mara tatu) kisha mguu wa kushoto hivyohivyo.



## Hatua ya 11 – Elekea kibla na uombe dua baada ya udhu

أشهد أن لا إله إلا الله، وحده، لا شريك له، وأشهد أن محمدًا عبده ورسوله.

***"Ash-hadu an la ilaha  illal lahu wa ash-hadu anna Muhammadan 'abduhu wa rasuluh."***

اللهم اجعلني من التوابين، واجعلني من المتطهرين.

"***Allahuma j'alnee mina tawabeen waj-'alnee minal mutatahireen***"

Kufikia hatua hii hapa itakua udhu wako umekamilika.

## Vitanguaji udhu

1. Kila chenye kutoka kwenye mojawapo ya njia mbili, mfano wa mkojo, choo, upepo (kushuta) kwa kauli yake Mtume ﷺ (Mwenyezi Mungu hakubali Swala ya mmoja wenu akitokwa na hadathi mpaka atawadhe) [Imepokewa na Muslim.].
2. kulala usingizi mzito ambao mtu hafahamu chochote. Na hi inaingia hapa, kama kukosa fahamu, na kupotezwa fahamu kikamilifu.
3. Kula nyama ya ngamia, kwa hadithi ya Jabir bin samurah kwamba mtu alimuuliza Mtume ﷺ: (Je, tutawadhe kwa kula nyama za ngamia? Akasema: (Ndio) [Imepokewa na Muslim.]
4. kugusa tupu kwa mkono bila ya kizuizi, kwa hadithi iliyo pokelewa na busra binti swafawan (RA) kuwa alimsikia mtume ﷺ akisema (mwenye kugusa tupu yake na atawadhe) [ Imepokewa na Abu Daud.]

# KUTAYAMAMU

Mwenyezi Mungu asema: “Na mkiwa wagonjwa au safarini, au mmoja wenu ametoka chooni au mmeingiliana na wanawake, na hamkupata maji, basi tayamamuni mchanga ulio safi.”

## Wakati Gani Tunatayammam?

i. Yanapokosekana maji ya kutosha kwa ajili ya udhu, au kuoga josho la kisharia.

ii. Tunapohofia kuwa kuyafikia maji kutatusababishia madhara juu ya nafsi, au mke na watoto au mali yenye kufungamana nasi.

iii. Ikiwa kuyapata maji au kuyatumia kutasababisha tabu na mashaka makubwa, ikiwemo madhila na uvunjifu wa heshima.

iv. Ufinyu wa muda katika kutafuta maji au kuyatumia kwa kiasi kwamba muda wa Swala utatupita.

v. Iwapo maji yatatosheleza tu kuondosha najisi mwilini na kwenye mavazi.2

## Tutatayammam Kwa Kutumia Vitu Gani?

i. **Udongo na mchanga.**

ii. **Mawe na miamba.**

iii. **Changarawe, na vinginevyo vinavyoitwa ardhi.**

## Vitenguzi Vya Tayammam:

Vitenguzi vya udhu hutumika kama vitenguzi vya tayammam, zaidi ya hapo ni kutoweka kwa udhuru uliyosababisha kufanyika kwa tayammam hiyo.


## Jinsi Ya Kufanya Tayammam:

**Kwanza:** Nia, nayo ni kukusudia moyoni kuwa: Ninatayammam badala ya udhu au josho kwa ajili ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

**Pili:** Kupiga mara moja juu ya ardhi kwa vitanga viwili, kama inavyoonekana katika picha



**Tatu:** Kupaka paji la uso kwa kutumia viganja viwili, kuanzia kwenye maoteo ya nywele mpaka kwenye nyusi pamoja na upande wa juu wa pua, na ni lazima kupaka kuanzia juu kwenda chini, kama inavyoonekana katika picha



**Nne:** Kupaka juu ya kitanga cha mkono wa kulia kwa kutumia kitanga cha mkono wa kushoto kuanzia kwenye kiwiko mpaka kwenye ncha za vidole, na lazima kupaka kuanzia juu kwenda chini, kama inavyoonekana katika picha



**Tano:** Kupaka juu ya kitanga cha mkono wa kushoto kwa kutumia kitanga cha mkono wa kulia kuanzia kwenye kiwiko mpaka kwenye ncha za vidole, na lazima kupaka kuanzia juu kwenda chini, kama inavyoonekana katika picha



# Mas'ala Mbalimbali Kuhusu Tayammam:

i. Ni wajibu kupiga juu ya ardhi, wala haitoshi kuweka tu mkono juu yake.

ii. Haisihi kutayammam kwa ajili ya faradhi ambayo bado wakati wake haujaingia.

iii. Tukitayammam kwa ajili ya Swala ambayo tayari muda wake umeshaingia na ikawa tayammam yetu haijatenguka wala udhuru uliyotusababisha tutayammam haujatoweka; hali hiyo ikaendelea mpaka ukaingia wakati wa sala nyingine, basi hapo tunaruhusiwa kusali Swala hii ya sasa kwa tayammam hiyo, madamu tu tunajua kuwa udhuru hautotoweka mpaka mwisho wa wakati.

Akitayammam badala ya josho, kisha akapatwa na hadathi ndogo, basi kwa mujibu wa ihtiyati atatakiwa kutayammam tena upya badala ya josho kisha achukuwe udhu, kama itawezekana. Kama haiwezekani basi atatayammam mara ya pili badala ya udhu

# Hedhi, inayofanana na hedhi na nifasi

## Hedhi

Ni damu inayotoka kwenye uzao wa mwanamke katika muda maalumu kama ada yake

## Damu ya istihadhah

### Maana ya istihadhah

Istihadhah

Ni kutiririka damu kutoka kwenye tupu ya mwanamke ikawa haikomi kabisa au ikatike kwa kipindi kichache.

## Tofauti baina ya damu ya hedhi na ya istihadhah

| Damu ya istihadhah | Damu ya hedhi |
|---|---|
| Nyekundu nyepesi | Nyeusi nzito |
| Haina harufu | Ina harufu mbaya yenye kuchukiza |
| Inaganda (inashikana) | Haigandi (haishikani) |
| Inatoka kwenye kishipa cha uzao cha karibu | Inatoka mwisho wa uzao |
| Damu ya kuashiria kasoro, ugonjwa na uharibikaji | Damu ya afya na ya kawaida |
| Haina wakati maalumu | Inatoka wakati maalumu |

## Hali za ailye kwenye istihadhah

## Hali ya kwanza: awe na ada inayojulikana ya siku zake za hedhi kabla ya kujiwa na istihadhah:

Huyo atahesabu siku za kadiri ya ada yake kuwa ni hedhi na zinazosalia katika mwezi ni istihadhah, kwa hadithi ya 'Aishah t kwamba Fatimah binti Abi Hubaish t alisema: (Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mimi sitwahiriki, je niache kuswali? Mtume akamwambia "La, hiko ni kishipa. Lakini acha kuswali kadiri ya siku zako za kuingia hedhini, kisha oga na uswali") [ Imepokewa na Bukhari.].

## Hali ya pili: Asiwe na ada inayojulikana, lakini anaweza kupambanua baina ya damu ya hedhi na damu ya istuhadhah:

Basi huyu atatumia upambanuzi wake, kwa ilivyothubutu kwamba Fatimah binti Hubaish t alikuwa kwenye damu ya istihadha, Mtume akamwambia: (Ikiwa ni damu ya hedhi, basi hiyo ni damu nyeusi inayojulikana. ikija, acha kuswali, na ikija ile nyingine tawadha na uswali, kwani damu hiyo ni kishipa) [ Imepokewa na Abu Daud.].

## Hali ya tatu: Asiwe na ada maalumu na asiweze kupambanua:

Basi huyo atatumia ada za wengi wa wanawake, hivyo basi hedhi itakuwa ni siku sita au saba katika kila mwezi, ataanzia mwanzo wa kipindi anapoona damu, na siku zilizosalia zitahesabiwa ni istihadha. Hii ni kwa kauli yake Mtume ﷺ kumwambia Hamnah binti Jahsh t: (Basi hesabu kuwa wewe uko hedhini kwa siku sita au siku saba, uhakika unajulikana na Mwenyezi Mungu, mpaka ukiona kuwa umetwahirika na umetakasika, swali kwa masiku ishirini na tatu au masiku ishirini na nne na michana yake, na ufunge, kwani hilo linakutosheleza. Na ufanye hivyo katika kila mwezi, kama wanavyohidhi wanawake na kama wanavyotwahirika wanawake wengine, kulingana na nyakati zao za hedhi na utwahara) [ Imepokewa na Abu Daud.]

## Hali ya nne: Awe na ada maalumu na aweze kupambanua:

Huyu atazingatia ada na siyo kupambanua, kwa kuwa ada ina udhibiti zaidi kwa mwanamke. Na anaposahau ada yake basi atatumia upambanuzi.

### Maelezo

1. Iwapo mwanamke anajua wakati wa hedhi yake, lakini akawa amesahau idadi ya siku zake za hedhi, basi atashika hesabu ya ada ya wengi wa wanawake.
2. Iwapo mwanamke anajua idadi ya siku zake za hedhi, lakini akawa amesahau wakati wa hedhi yake, iwapo ni mwanzo wa mwezi au ni mwisho wake, atahesabu mwanzo wa mwezi idadi ya siku zake za hedhi. Akisema kuwa yamjia mwanzo wa mwezi lakini hawezi kujuwa ni lini wakati wake, atashika hesabu kuanzia mwanzo wa nusu idadi ya siku ilipokuwa hedhi yake ikimjia, kwa kuwa nusu ya mwezi ndio kadiri iliyo karibu zaidi ya kudhibiti wakati wake.

3. Kikipita kipindi cha hedhi, na mwanamke yuko kwenye istihadhah basi ataoga kisha atafunga kitambaa kwenye tupu yake. Na hukumu yake itakuwa ni ile ya twahara, ataswali na atafunga, na haitamdhuru damu itakayomtoka baada ya kutawadha kwa kuwa ana udhuru, na atafanya mojawapo ya mambo matatu katika twahara:

a. Atawadhe kwa kila Swala baada ya wakati kuingia. Hilo ni baada ya kuosha tupu yake na kuifunga kitambaa, kwa kauli ya Mtume ﷺ kumwambia Fatimah binti Hubaish t: (Kisha tawadha kwa kila Swala na uswali) [ Imepokewa na Abu Daud.].

b. Aicheleweshe Adhuhuri mpaka kabla ya Alasiri, kisha aoge na aswali Adhuhuri na Alasiri, na atafanya hivi katika Swala nyingine. Hii ni kwa neno lake Mtume ﷺ kumwambia Hamnah binti Jahsh t: (Na ukiweza kuchelewesha Adhuhuri na kuitanguliza Alasiri, ukaoga na ukakusanya baina ya Swala mbili: Adhuhuri na Alasiri, na ukachelewesha Magharibi na akaianguliza Swala ya Isha, kisha uoge na ukusanye Swala mbili, basi fanya hivyo. Na ukiweza kuoga wakati wa wa swala ya Alfajiri basi fanya hivyo, na ufunge, kama waeza kufunga) [ Imepokewa na Abu Daud.].

4. Mwanamke akitokwa na damu kwa sababu yoyote ile, kama operesheni, na ikatiririka, basi yeye ni mojawapo wa hali mbili:

a. Ijulikane kuwa hatapata hedhi. Huyu hazipitishwi kwake hukumu za istihadhah, wala haachi kuswali wakati wowote, na ile damu ni ya ugonjwa na kuharibika kwa kitu, na atatawadha kwa kila Swala.

b. Ijulikane kuwa yeye inamkinika kuingia hedhini. Huyu hukumu yake ni ya istihadhah.

5. nafaa kumuingilia mwanamke aliye kwenye istihadhah.kwa kuwa Sheria haikumkataza.

## Nifasi

### Maana ya Nifasi

## Nifasi

Ni damu inayotoka kwenye uzao wa mwanamke kwa sababu ya kuzaa

### Muda wa Nifasi

Hakuna mpaka wa uchache wa nifasi. Ama wingi wake kwa kawaida ya wengi ni siku arubaini, isipokuwa akiona utwahara kabla ya hapo, Basi ataoga na aswali.

Ingia katika kiungo kifuatacho upate maelezo zaidi:
Ghuslu - Muda Wa Kutwaharika Na Damu Ya Nifasi

### Miongoni mwa hukumu za nifasi

1. Mwanamke akizaa na asione damu- na hii ni hali ya nadra sana- atatawadha na ataswali, na halazimiki kuoga.
2. Damu ikipita siku arubaini, na ikawa ada yake ni kukatika kwa kumalizika siku ya arubaini, au zikadhihiri alama za kukaribia kukatika, atangojea mpaka ikatike. Iwapo damu itaendelea, basi yeye ana istihadhah na itamthibitikia yeye hukumu za istihadhah.
3. Akitwahirika kabla ya siku ya arubaini, kisha damu ikamrudia ndani ya siku arubaini itamlazimu aangalie: .
a. Akijua kuwa ni damu ya nifasi, basi ni damu ya nifasi.
b. Na akijua kuwa si damu ya nifasi, basi hukumu yake ni kuwa yuko katika twahara.
4. Haithubutu damu kuwa ni ya nifasi isipokuwa akiwa amezaa kitu chenye umbo la binadamu, akiwa amezaa tisha- naye ni mtoto aliyetoka kwenye uzao wa mwanamke kabla ya umbo lake kukamilika- ambalo halijafafanuka kwake umbile la binadamu. Nalo lina hali tatu:
a. Iwe ni kabla ya siku arubaini za kwanza (za kushika mimba). Bila ya hivyo, hii itakuwa ni damu iliyoharibika, hivyo basi ataswali na atafunga.
b. Iwe ni baada ya siku thamanini. Na hii ni damu ya nifasi.
c. Iwe muda wake wa kukaa matumboni ni baina ya siku arubaini na thamanini. Na hii itatazamwa: Iwapo imeonesha alama ya kuwa

ni kiumbe, basi hiyo ni damu ya nifasi. ikitokuwa hivyo, basi ni damu iliyoharibika

## Yanayoharamishwa kwa ajili ya hedhi na nifasi

### 1. Kujamiana

Kwa neno lake Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Na wanakuuliza juu ya hedhi. Waambie, huo ni uchafu basi jitengeni na wanawake wakati wa hedhi.wala msiwaingilie mpaka watahirike. Wakisha twahirika basi waendeni alivyo kuamrisheni mwenyezi mugnu.} [2: 222]

Na kwa kauli ya Mtume ﷺ ilipoteremka aya hii: (Fanyeni kila kitu isipokuwa kuundama) [ Imepokewa na Muslim.].

### Maelezo

1. Mwenye kumuingilia mkewe na hali yuko katika hedhi hupata dhambi na itamlazimu kafara na huyo mke pia atoe kafara iwapo aliridhia.

Na kafara ni kutoa sadaka kadiri ya dinari moja au nusu dinari ya dhahabu, kwa hadithi ya Ibnu Abbas kumpokea Mtume ﷺ juu ya mtu anayemuingilia mkewe na hali yuko kwenye hedhi kuwa alisema: (Atatoa sadaka Dinari moja au nusu dinari) [ Imepokewa na Muslim.].

Dinari moja ni grama nne na robo za dhahabu.

2. Aliyoko hedhini akiingia twaharani, haifai kwa mumewe kumuundama (kumuingilia) mpaka aoge, kwa neno la Mwenyezi Mungu Aliyetukuka {Na msiwakaribie mpaka watwahirike} yaani: kutokana na damu.

Kisha akasema: {wakijitwahirisha} yaani: wakaoga.

Kisha akasema {Wajieni kupitia pale alipowaamrisha nyinyi Mwenyezi Mungu} [2: 222], yaani: kuundama.

### 2.Kuswali

Kwa neno lake Mtume ﷺ: (Ikija hedhi acha kuswali, na ikiondoka Safisha damu kwa kuoga kisha uswali) [ Imepokewa na Abu Daud.].

### Maelezo

1. Mwanamke haimlazimu kulipa swala akitwahirika, Kwa hadithi iliyothubutu kutoka kwa ‹Aishaah t kuwa aliulizwa juu ya aliyekuwa na hedhi kulipa Saumu na kutolipa Swala, akasema: (Tulikuwa tukipatikana na hilo tukiamrishwa kulipa saumu na hatukuwa tukiamrishwa kulipa Swala) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

2. Iwapo mwenye hedhi atawahi rakaa nzima ya wakati wa Swala, itamlazimu aswali, iwe ni rakaa ya mwanzo ya wakati au ya mwisho wake. Ikiwa atawahi sehemu ya wakati ambayo haikundukii rakaa moja, basi haimlazimu kuswali, kwa kauli ya Mtume ﷺ: (Mwenye kuwahi rakaa moja ya Swala amewahi swala) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.]

### 3. Kufunga Saumu

Kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Kwani akiingia katika hedhi si ataacha kuswali na kufunga? Wakasema (wanawake): “Ndiyo”) [ Imepokewa na Bukhari.].

### Maelezo

Akitwahirika mwenye hedhi kabla ya Alfajiri na akafunga, basi Saumu yake itakuwa sahihi, ingawa hakuoga mpaka baada ya Alfajiri

### 4. Kushika Msahafu

Kwaneno lake Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Hawaigusi isipokuwa walitwahirishwa} [56: 79]

Na kwa neno lake Mtume (Hawagusi Mswahafu ila aliye twahara) [ Imepokewa na Malik katika Muwatta’].

### 5. Kutufu Alkaaba

Kwa neno la Mtume ﷺ kumwambia ‹Aishah t: (Fanya kile anachokifanya mwenye kuhiji isipokuwa usitufu Alkaaba mpaka uwe twahara) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.]
na kwa haditi ya Ibn ‘Abbas t alisema: (Wameamrishwa watu iwe mwisho wa kukutana kwao na Alkaaba ni kutufu, isipokuwa mwanamke mwenye hedhi amehafifishiwa hilo) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.]

### 6. Kukaa msikitini isipokuwa mpita njia

Kwa neno lake Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Enyi mlioamini! Msikaribie swala hali mmelewa, mpaka myajue mnayo yasema, wala hali mna janaba isipo kuwa mmo safarini mpaka muoge} [4: 43]
na kwa neno la Mtume ﷺ (Mimi simhalalishii msikiti mwenye hedhi wala mwenye janaba)

### Maelezo

1. Si makosa kwa mwenye hedhi kupita msikitini akijihifadhi na asichelee kuuchafua msikiti, kwa ujumla wa maneno ya Mwenyezi Mungu Aliyetuka: {Isipokuwa wapita njia} [4: 43]
2. Ni haramu kwa mwenye hedhi kukaa kwenye eneo la kuswalia Idi, kwa neno lake Mtume ﷺ (Na wajiepushe na kuhudhuria mahali pa kuswali Idi) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

### 7.Talaka

Ni haramu kwa mume kumuacha mkewe akiwa na hedhi, kwa neno lake mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Ewe Nabii mkiwataliki wanawake, watalikini mkizingatia eda lao } [65: 1].
Yaani waelekee kwenye eda maalumu wakati wa kuachwa.
Na talaka ya mwenye hedhi inapita ingawa ni haramu na ni uzushi katika Dini.
Ingia katika kiungo kifuatacho upate maelezo zaidi:
Ghuslu - Vipi Kukoga Janabah, Nifaas Na Hedhi

# SWALAH

Ni kumuabudu Mwenyezi Mungu  kwa maneno na vitendo maalumu, vinavyoanzia kwa takbiri na vinavyomalizikia kwa kupiga salamu.

## Hukumu ya Swala

Swala tano ni wajibu kulingana na Qur›ani, Sunna na umoja wa wanavyuoni:

1. Qur'ani:

Anasema Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Na simamisheni Swala na toeni Zaka na rukuuni pamoja na wenye kurukuu} [2: 43].

2. Sunna:

Amesema ﷺ: (Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano: kushuhudia kuwa hapana mola isipokuwa Mwenyezi Mungu na kwamba Muhammad ni mja Wake na mtume wake, na kusimamisha Swala, nakutoa Zaka, nakuhiji Alkaba na kufunga mwezi wa Ramadhani) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

- Na imepokewa kutoka kwa Twalhah bin 'Ubeidillah kwamba mtu mmoja alimuuliza Mtume ﷺ kuhusu Uislamu, akasema ﷺ: (Ni Swala tano mchana na usiku. Akasema: "Je, kuna nyingine zinazonilazimu sizizokuwa hizo?" Akasema: La, isipokuwa ukijitolea) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

3. Umoja wa wanavyuoni:

Umma kwa umoja wao wamekubaliana juu ya uwajibu wa Swala tano kipindi cha mchana na usiku.

## Hukumu ya mwenye kuacha Swala

### 1. Mwenye kuacha Swala kwa kukanusha uwajibu wake:

Atafahamishwa akiwa hajui. Akiendelea kukanusha kwake, basi yeye ni kafiri, mkanushaji wa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na umoja wa Waislamu.

### 2. Mwenye kuacha Swala kwa uvivu:

Mwenye kuacha Swala kwa kukusudia na uvivu atakuwa amekufuru. Na ni juu ya kiongozi amlinganie kuswali na amuorodheshee toba kwa muda wa siku tatu. Basi akitubia ni sawa, na akitotubia atamuua kwa kuwa ameritadi. Hii ni kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Ahadi iliyoko baina ya sisi na wao ni Swala. Yoyote yule atakayeiacha basi atakuwa amekufuru ) [ Imepokewa na Tirmidhi.], na kauli yake ﷺ: (Hakika baina ya mtu na ushirikina na ukafiri ni kuacha Swala) [ Imepokewa na Muslim.].

Swala ya mtoto

Mtoto anaamrishwa kuswali akifika miaka saba, kwa kumzoeza, na anapigwa kwa kuiacha afikapo miaka kumi kipigo kisichoumiza. Amesema Mtume ﷺ: (Waamrisheni watoto wenu kuswali wakiwa ni vijana wa miaka saba, na wapigeni kwa kuiacha swala wakiwa ni vijana wa miaka kumi)) [ Imepokewa na Abu Daud.].

# Masharti ya kufanya Swala iwe sahihi

## Kwanza: kuingia wakati

Swala ya faradhi ina wakati ambao haiswihi kabla yake, wala baada yake isipokuwa kwa dharura. Asema Mwenyezi Mungu aliyetukuka: { Hakika Swala kwa Waumini ni faradhi iliyo wekewa nyakati maalum} [4: 103],

yaani imefaradhiwa katika vipindi maalumu.
Nyakati za Swala ni: .

### 1. Wakati wa Alfajiri:

Ni kuanzia kutoka alfajiri ya kweli, nao ni ule weupe unaokuwa kwenye pambizo upande wa Mashariki, mpaka kuchomoza jua.

### 2. Wakati wa Adhuhuri:

Ni kuanzia kupinduka jua mpaka kivuli cha kitu kiwe mfano wake, baada ya kile kivuli cha kupinduka jua. Hivyo ni kwamba jua likichomoza kitu kinachosimama huwa na kivuli upande wa magharibi, kisha kivuli hiko huenda kikipungua kila jua likipanda mpaka kivuli kisimame. Kisha kivuli kinaanza kuongezeka, na ongezeko hili lianzapo hua ndio wakati wa kupinduka.

### 3. Wakati wa Alasiri:

Ni kuanzia wakati wa Adhuhuri kuisha mpaka kivuli cha kitu kiwe ni mara mbili yake baada ya kivuli cha kupinduka jua.

### 4. Wakati wa Magharibi:

Ni kuanzia jua linapozama mpaka yapotee mawingu mekundu, nayo ni ule mwangaza mwekundu unaokuwa kwenye pembe za mbingu pale jua linapozama.

### 5. Wakati wa Isha:

Ni kuanzia kipindi cha Magharibi mpaka nusu ya usiku, kwa neno lake ﷺ: (Wakati wa Swala ya Isha ni mpaka usiku wa kati)
[ Imepokewa na Muslim.].
Na katika zama hizi, inawezekana kujua nyakati za Swala kwa urahisi kwa njia ya kuweka jaduali za kujulisha nyakati.

Yasiofaa

- Kuswali na nguo ya kubana yenye kusifu uchi wa mtu, au nguo nyembamba yenye kuonyesha, au kuswali na huku akiwa tupu yake inaonekana, au na isbaal nao ni mtu kuswali na nguo yake imevuka vi fundoni.
- Kuswali na nguo yenye picha, au kuswali sehemu zilowekwa picha za roho, au kuswalia mswala wenye picha na michoro.

- Kuswali katika Msikiti wenye Makaburi, kwa neno lake Mtume ﷺ (Jueni kuwa watu walio kuwa kabla yenu wakiyafanya makaburi ya manabii wao na watuwema wao misikiti, basi musiyafanye makaburi yeni misikiti mimi nawakataza hilo) [ Imepokewa na Muslim.]

Faida

1. Mwenye kuwahi rakaa moja kabla ya kutoka wakati huwa amewahi Swala, kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Mwenye kuwahi rakaa moja ya Swala huwa amewahi Swala) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

2. Ni lazima kutekeleza Swala kwa haraka iwapo wakati wake umepita kwa kulala au kwa kusahau, kwa neno lake Mtume ﷺ: (Mwenye kuisahau Swala basi ni juu yake aiswali anapoikumbuka, hakuna kafara yake isipokuwa hiyo) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.]

## Pili: Kutwahirika na hadathi

### 1. Kutwahirika na hadathi ndogo (tukio la kutokuwa na udhu):

Nako kunapatikana kwa kutawadha. Mtume ﷺ anasema: (Mwenyezi Mungu hatakubali Swala ya mmoja wenu akitokewa na tukio la kutokuwa na udhu mpaka atawadhe) [ Imepokewa na Bukhari].

### 2. Kutwahirika na hadathi kubwa:

nako kunapatikana kwa kuoga, kwa neno la mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Na mkiwa na janaba jitwahirisheni} [5: 6].

Na yoyote atakayekumbuka akiwa katika Swala kuwa hana udhu au ametokewa na jambo la kuharibu udhu katikati ya Swala, basi Swala yake itatanguka Na itamlazimu ajitoe Swalani ili ajitwahirishe na bila ya kutoa Salamu, kwa kuwa swala

ishatanguka na bado haijamalizika, na utoaji salamu ndio mwisho wa Swala.

## Tatu: Utwahara wa Nguo, mwili na mahali

### 1. Utwahara wa nguo,

kwa neno lake Mwenyezoi Mungu aliyetukuka: {Na nguo zako twahirisha} [74: 4].

### 2. Utwahara wa mwili,

kwa ilivyothubutu kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliipita kwenye kaburi mbili akasema: (Hakika wawili hawa wanaadhibiwa. Na hawaadhibiwi kwa jambo kubwa. Ama huyu alikuwahajiepushi [ Laa yastanzihu min al-baul: hajiepushi na hajikingi na mkojo.] na mkojo usimuingie) [ Imepokewa na Abu Daud.].

### 3. Utwahara wa mahali,

kwa hadithi ya mbedui aliyekojoa msikitini. Mtume ﷺ alisema: (Muacheni na umwagieni [ Hariiquu: mwageni.] mkojo wake ndoo [ Dhanuub: ndoo kubwa iliyojaa maji.] ya maji) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

### Swala na Najisi

Mwenye kuswali naye ana najisi bila ya kuijua au akaisahau, basi Swala yake ni sahihi. Kwa kuwa ilithubutu kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliswali akavua viatu vyake, na watu wakavua viatu vyao. Alipoondoka alisema ﷺ: (kwa nini mlivua viatu vyenu? Wakasema: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Tulikuona ukivua viatu vyako na sisi tukavua”. Mtume akasema: “Jibrili alinijia akanipasha habari kwamba viatu vina uchafu. Basi anapokuja mmoja wenu msikitini, avigeuze viatu vyake avitazame. Akiona kuwa vina uchafu,

basi na avisugue chini kisha aswali navyo) [ Imepokewa na Abu Daud.].

Yoyote atakayejua kuwa ana najisi akiwa katikati ya Swala, itamlazimu kuiondoa, kisha aendelee na Swala yake na ajengee juu ya kile alichokiswali, kwa hadithi iliyotangulia. Akitoweza kuiondoa, swala yake itatanguka.

### Ardhi yote ni Msikiti

Ardhi yote ni msikiti, kwa kuwa kuswali hapo inafaa. Mtume ﷺ amesema: (Nimefanyiwa ardhi kuwa ni mahali pa kuswali na mahali pakujitwahirishia. Basi mtu yoyote miongoni mwa umma wangu aliyeingiliwa na kipindi cha Swala na aswali) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Kinachovuliwa hapo ni kuswali kwenye sehemu zilizokatazwa, kama vile kuswali makaburini (Kinachovuliwa hapo ni Swala ya maiti.) na chooni, kwa kuwa Mtume ﷺ alisema: (Ardhi yote ni mahali pa kuswali, isipokuwa makaburini na chooni) [ Imepokewa na Tirmidhi.].

Na pia sehemu ya malazi ya ngamia kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Musiswali katika malazi ya ngamia) [ Imepokewa na Tirmidhi.]. Na hapo ni mahali pa ngamia kulala na kukusanyika.

## Nne: Kusitiri tupu

Tupu ya mwanamume: ni kuanzia kitovuni hadi gotini.
Tupu ya mwanamke: ni mwili wake wote isipokuwa uso na vitanga vya mikono.

### Kufinika mabega

Inamlazimu mwenye kuswali avae nguo yenye kufinika mabega yake na shingo yake, kwa kuwa Mtume alisema: (Asiswali mmoja wenu kwa nguo moja bila ya kuwa imefinika mabega yake) [ Imepokewa na Tirmidhi.].

isipokuwa yeye hakuwa akiswali juu yake Swala za faradhi) [ Imepokewa na Tirmidhi.].

## Tano: Kuelekea Kibla

Na kibla ni alkaaba tukufu

Mwenyezi Mungu Aliyetukuka Amesemna: { Elekeza uso wako upande wa msikiti wa Haram. Na popote mlipo, elekezeni nyuso zenu upande wake} {Al-Baqara: 144}.

Na inalazimu kuchunga baadhi ya mambo:

1. La wajibu kwa mwenye kuswali ndani ya msikiti wa Haram aielekee alkaba yenyewe. Ama yule anayeswali akiwa mbali na Alkaaba, basi ataelekea upande wa hiyo Alkaba na sio kuielekea yenyewe, kwa kuwa hawezi kuielekea yenyewe. Kwa hivyo, Mtume ﷺ alisema: (baina ya mashariki na magharibi ni kibla) [ Imepokewa na Tirmidhi].

2. Swala ya Sunna kwa aliyepanda mnyama, kibla chake ni ule upande ambao kile kipando kinaelekea, kwa kuwa ilithubutu kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akiswali [ Yusabbihu: anaswali Swala ya Sunna.] juu ya kipando chake akielekea popote pale kile kipando kinapoelekea, na alikiswali witri juu yake, isipokuwa yeye hakuwa akiswali juu yake Swala za faradhi) [ Imepokewa na Abu Daud.].

- Asiyejua Kibla Atafanya Nini?

Asiyejua kibla akiwa kwenye jengo au mahali penye watu walio karibu, atauliza au atajijulisha kibla kwa vibla vya misikiti au dira au jua au mwezi au vinginevyo. Akitoweza kujua basi atajitahidi na atafuata lile lenye nguvu katika dhana yake, kwa neno lake Mwenyezi Mungu: {Muogopeni Mwenyezi Mungu vile mnavyoweza} [64: 16].

# Namna ya kuswali

Amesema Mtume ﷺ (Swalini kama munavoniona mimi nikiswali) [ Imepokewa na Bukhari]


Aisha alipokewa kwamba alisema: (Mtume ﷺ alikuwa akifungua Swalah kwa Takbiri na kisomo cha "Alhamdu lillaahi Rabbil 'aalamiin", na alikuwa akirukuu hakiinamishi kichwa chake na wala hakisimamishi sawa, bali alikikiweka baina ya hali hizo mbili. Na alikuwa akiinua kichwa chake kutoka kwenye rukuu, hasujudu mpaka alingane katika kusimama. Na alikuwa akisoma Atahiyatu katika kila rakaa mbili, na alikuwa akikalia mguu wake wa kushoto na akiusimamisha mguu wake wa kulia. Na alikuwa akikataza mkao wa Shetani (kukaa kama shetani) na alikikataza mtu kuiweka chini mikono yake katika kukaa kama vile mnyama wa kuwinda, na alikuwa akihitimisha Swala yake kwa kupiga Salamu) [ Imepokewa na Muslim.].



1.**Nia:** - Anayetaka kuswali atasimama hali ya kuelekea Kibla na kujihisi kuwa amesimama mbele ya Mwenyezi Mungu Aliyetukuka, hali ya kuwa ni mnyenyekevu katika kuswali kwake.

- Kisha anuilia kuswali moyoni mwake.na nia pahali pake ni moyoni, na haifai kuitemka nia kwani kufanya hivyo ni uzushi.Amesema Mtume (Hakika amali zote ni kwa nia na kila mtu hulipwa kwa alilo nuiliya) [Imepokewa na Bukhari.na muslim. ]

**2. Takbira ya kuhirimia:** Yenyewe husomwa mara baada ya nia kwa kusema **"Allahu Akbar".** Ambapo ni sunna



kuinua mikono mpaka usawa wa masikio, ni lazima uanzaji wa kuinua mikonouende sanjari na uanzaji wa tamko, na umalizike sanjari na tamko hilo,



3. Soma dua ya kufungua sala

سُبْحانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ، وَتَبارَكَ اسْمُكَ، وَتَعَالَى جَدُّكَ، وَلاَ إِلَهَ غَيْرُكَ

Subhaanaka Allaahumma wa bihamdika, wa tabaarakasmuka, wa ta'aalaa jadduka, wa laa 'ilaaha ghayruka.

Kisha usome *Ta'awwudh* halafu usome *bismillah*.

اعوذ بالله من الشيطان الرجيم

auzu billahi minash shaitan rajeem

بسم الله الرحمن الرحيم

bismillah hir rahman nir Raheem

Baada ya hapa utasoma suratul fatiha

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَۙ(١) الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِۙ(٢) مٰلِكِ يَوْمِ الدِّيْنِؕ(٣) اِيَّاكَ نَعْبُدُ وَ اِيَّاكَ نَسْتَعِيْنُؕ(٤) اِهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيْمَۙ(٥) صِرَاطَ الَّذِيْنَ اَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ الْمَغْضُوْبِ عَلَيْهِمْ وَ لَا الضَّآلِّيْنَ (٧

Alhamdu lillaahi Rabbil ‘aalameen Ar-Rahmaanir-Raheem Maaliki Yawmid-Deen Iyyaaka na’budu wa Iyyaaka nasta’een Ihdinas-Siraatal-Mustaqeem Siraatal-lazeena an’amta ‘alaihim ghayril-maghdoobi ‘alaihim wa lad-daaalleen

BAADA ya Fatiha soma sura yoyote utakayoweza


Kwa mfano unaweza kusoma suratul ikhlas:

Surah Ikhlas:

بسم الله الرحمن الرحيم

قل هوا لله أحد،الله الصمد، لم يلد و لم يولد، و لم يكن له كفوا أحد

Bismillah hir Rahman nir Rahim Qul Huwallahu ahad. Allahussamad. Lam yalid wa lam yu-lad. Wa lam yakun lahu kufuwan ahad.




**4.** Kisha useme Allahu Akbar halafu urukuu na kusema mara tatu:. **Rukuu:** Baada ya kumaliza kisomo, inama kwa ajili ya rukuu na useme: سُبْحَانَ رَبِّيَ الْعَظِيمِ **“Sub’hana rabbiyal Adhiim wabihamdihi**," kama inavyoonekana katika picha

5. Kisha inua kichwa chako toka kwenye rukuu usimame ukiwa mnyoofu, kisha useme: سَمِعَ اللهُّ لِمَنْ حَمِدَه **“Samiallahu liman hamidah”** رَبَّنَا وَلَكَ الْحَمْد Rabbana alkali hamd. kama inavyoonekana katika picha.



Kisha utasubiri kidogo kabla ya kwenda kusujudu.

6. Kisha useme Allahu Akbar kisha utaporomoka kwenda kusujudu kwa kuweka viungo saba vya sijda juu ya ardhi na kusema:



سُبْحَانَ رَبِّيَ الأَعْلَى Subhana Rabbiyal A’la
Kisha tunainua kichwa kutoka kwenye sijda ya kwanza na kutulia kidogo, kisha tunasema: **“Allahu Akbar”.** Kisha tunakwenda kusujudu kwa mara nyingine kwa kufanya kama tulivyofanya katika sijda ya kwanza na kusoma tuliyosoma katika sijda ya kwanza, kama inavyoonekana katika picha.

7. Kisha useme Allahu Akbar halafu ukae kitako useme:


رب اغفر لي ,
Rabbighfir li

8. Hapa tunasoma Tashahhud kimyakimya kwa kusema:



التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ وَالصَّلَوَاتُ وَالطَّيِّبَاتُ، السَّلاَمُ عَلَيْكَ أَيُّهَا
النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللهِ وَبَرَكَاتُهُ، السَّلاَمُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ
اللهِ الصَّالِحِينَ، أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ
مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ

Attahiyat lillahi wa salawatu wa’t-tayyibat, as-salamu ‘alayka ayyuha’n-Nabiyyu wa rahmat-Allahi wa barakatuhu. As-



salamu ‘alayna wa ‘alaa ‘ibad-Illah is-saliheen. ashhadu alla ilaha illallah wa ashhadu anna muhammadan ‘abduhu wa rasuluhu

ٱللَّٰهُمَّ صَلِّ عَلَىٰ مُحَمَّدٍ وَعَلَىٰ آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ
عَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ وَعَلَىٰ آلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ ٱللَّٰهُمَّ
بَارِكْ عَلَىٰ مُحَمَّدٍ وَعَلَىٰ آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَىٰ
إِبْرَاهِيمَ وَعَلَىٰ آلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ

Allahumma salli ‘ala Muhammadin Wa ‘ala ali Muhammadin Kama sallaita ‘ala Ibrahima wa ‘ala ali Ibrahima wa barik ‘ala Muhammadin wa ‘ala ali Muhammadin Kama barakta ‘ ala Ibrahima Wa ‘ ala ali Ibrahima Fil a’lamina Innaka hamidun Majid.”

9. Toa salamu kwa kuelekeza uso wako kulia halafu kushoto kwa kusema:

السَّلاَمُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللهِ

Assalamu alaikum wa rahmatullah

Baada ya salamu itakua sala ishakwisha.

# Nguzo za Swala na Wajibu wake na Sunna zake

Nguzo za Swalah

Ni sehemu zake za kimsingi ambazo Swala inatokana nazo, kwa namna isiyofaa kuziacha kwa hali yoyote ile. Hazipomoki kwa kukusudia wala kwa kusahau isipokuwa katika hali ya kutoweza.

1. Kutia nia
2. Kusimama katika swala ya faradhi pamoja na kuweza
3. Takbiri ya kufungia Swala
4. Kusoma Fatiha
5. Kurukuu
6. Kuitadili kwa kulingana sawa baada ya kurukuu
7. Kusujudu kwa viungo saba
8. Kukaa baina ya sijida mbili
9. Kukaa kwa Atahiyatu ya mwisho.
10. Kusoma Atahiyatu
11. Kumswalia Mtume ﷺ katika Atahiyatu ya mwisho.
12. Kutoa salamu
13. Kujituliza katika nguzo zote
14. Kutungamanisha baina ya nguzo

### Atafanya nini mwenye kuacha nguzo moja miongoni mwa nguzo za Swalah?

### 1. Mwenye kuacha nguzo kwa kusudi Swala yake inabatilika na inamlazimu kuirudia.

### 2. Mwenye kuacha kwa kusahau, basi ni moja wa hali mbili:

a. Asikumbuke kuwa yeye ameiacha nguzo hii mpaka baada ya kuifika pale mahali pake katika rakaa iliyofuatia. Basi hapa ile rakaa iliyopita ambayo aliiacha nguzo hiyo haitahesabiwa, na ataifanya rakaa hii ndiyo badala ya rakaa aliyoisahau, kisha atasujudu sijida ya kusahau118.

- Mfano wake: Mtu alikumbuka katika rakaa ya pili katika kusoma Fatiha kuwa yeye alisahau kusoma Fatiha katika rakaa ya kwanza. Hapa ataifanya rakaa yake hii kuwa ndio rakaa yake ya kwanza na ile iliyotangulia ataipuuzwa.

b. akumbuke kuwa alisahau nguzo kwenye rakaa, kabla hajafika kwenye mahali pa nguzo hiyo katika rakaa inayofuata. Hapa itamlazimu kurudia nguzo hiyo kwa haraka pale anapokumbuka.

- Mfano wake: Mtu alisahau kurukuu kisha akasujudu alipomaliza kisomo chake, kisha akakumbuka alipokuwa hali ya kusujudu kuwa bado hajarukuu. Basi huyu itamlazimu asimame arukuu kisha akamilishe Swala yake.

## Pili: Mambo ya wajibu katika swalah

### Mambo ya wajibu katika swala

Ni yale yanayoungwaungwa kwa sijida ya sahau na yanapomoka kwa kuyasahau

1. Takbiri za kuhamia kutoka kwenye kitendo kwenda kwenye kingine.
2. Kusema SUBHANA RABIYAL ADHIIM “Kutakasika ni kwa Mola wangu Mkubwa”.
3. Kusema SAMI’A LLAHU LIMAN HAMIDA “Mwenyezi Mungu Amemsikia mwenye kumsifu” kwa imamu na kwa mswali pweke, ama maamuma hakuwekewa na Sheria kusema neno hilo.
4. Kusema RABBANAA LAKAL HAMDU “Mola wetu! Na sifa njema zote ni zako” katika kuitadili kutoka kwenye rukuu.
5. Kusema SUBHANA RABBIYAL A’LAA “Kutakasika ni kwa Mola wangu Aliye juu” katika sijida.
6. Kusema RABBIGH FIRLIY “Mola wangu ! nighufirie” baina ya sijida mbili.
7. Kukaa kikao cha Atahiyatu ya kwanza.
8. Kuleta Atahiyatu ya kwanza

### Atafanya nini mwenye kuacha jambo la wajibu miongoni mwa wajibu wa swalah ?

1. Mwenye kuiacha kwa kukusudia Swala yake inabatilika na itamlazimu kuirudia.
2. Mwenye kuiacha kwa kusahau, basi Swala yake ni sahihi, na atasujudu sijida mbili za sahau kabla hajapiga salamu.

## Tatu: Sunna za Swalah

Na kila kisichokuwa ni miongoni mwa masharti ya Swala, nguzo zake na mambo yake ya wajibu katika vile vilivyotajwa juu ya Namna ya Kuswali, basi hicho ni sunna ambao kuiacha hakuathiri katika usahihi wa Swala wala hailazimu kwa kuacha kusujudu sijida sahau.

Na sunna za Swala ni aina mbili:

### Kwanza: Sunnah za maneno

1. Dua ya ufunguzi wa Swala: Nayo ni dua inayosomwa kabla ya kusoma Fatiha.
2. Kuleta Audhu: nako ni kusema A'UDHU BILLAHI MINA SHETWANI RAJIIM (Najilinda kwa Mwenyezi Mungu kutokana na Shetani aliyefukuzwa kwenye rehema ya mwenyezi Mungu).
3. Kuleta bismillahi nako ni kusema BISMILLAHI RRAHMANI RRAHIM (Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu).
4. Tasbihi iliyo zaidi ya moja katika kurukuu na kusujudu.
5. Maneno ya ziada baada ya kusema RABBIGH FIRLIY (Mola wangu nighufirie) baina ya sijida mbili.
6. Kisomo cha ziada baada ya RABBANAA LAKAL HAMDU (Mola wetu! Na sifa njema zote ni zako) baada ya kuinuka kutoka kwenye rukuu.
7. Kisomo cha ziada baada ya Suratul Faatiha

### Pili: Sunnah za vitendo

Nazo ni nyingi miongoni mwazo ni:

1. kuinua mikono pamoja na takbiri ya kufungia Swala, wakati wa kurukuu, kuinuka kutoka kwenye rukuu wakati wa kuinuka kwenda kwenye rakaa ya tatu.
2. Kuweka mkono wa kulia juu ya wa kushoto wakati wa kusimama kabla ya kurukuu na baada yake.
3. Kuangalia mahali pa kusujudu.

4. Kuiepusha mikono iwe kando na tumbo na mbavu wakati wa kusujudu.
5. Kukaa kikao cha iftiraash: nacho ni kukaa hali ya kuinua nyayo za mguu wa kulia na kuvielekeza vidole vyake kibla, hali ya kuweka mguu wa kushoto chini na kuukalia. Kikao hiki kimesunniwa katika vikao vyote vya Swala isipokuwa kikao cha Atahiyatu ya mwisho ya Swala ambayo rakaa zake zinapita mbili.
6. kikao cha tawarruk: nacho ni kukaa hali ya kusimamisha nyayo za mguu wa kulia na kuzielekeza vidole vyake kibla, na kuziweka nyayo za mguu wa kushoto chini ya muundi wa mguu wa kulia na kuzitoa nyayo upande wa kulia na kukalia kitako kwa kujitegemeza kalio la upande wa kushoto. Kikao hiki ni sunna kwa Attahiyatu ya mwisho ya Swala inayozidi rakaa mbili.

Ingia katika kiungo kifuatacho upate maelezo zaidi:
Swalaah Za Sunnah Zinaswaliwa Rakaa Ngapi Ngapi?



Kikao cha iftiraash



Kikao cha tawarruk

# Swalah ya Janeza

## Swalah ya Maiti

### Nguzo za Swala ya maiti

1. Kusimama kwa anayeweza.
2. Takbiri nne..
3. Kusoma Fatiha.
4. Kumswalia Mtume ﷺ.
5. Kumuombea Maiti Dua
6. Kutugamanisha (kutaratibisha).
7. Kutoa Salamu.

### Sunnah za Swalah ya Maiti

1. Kuleta A›udhu..kabla ya kusoma.
2. Kujiombea dua mwenye kuswali na kuwaombea Waislamu.
3. Kusoma kwa siri.
4. Kuzifanya safu ziwe nyingi, ziwe tatu au zaidi.

### Namna ya kuswalia maiti(jeneza)

Atasimama imamu kwenye kichwa cha maiti iwapo ni mwanamume, na katikati ya maiti iwapo ni mwanamke. Na maamuma watasimama nyuma yake kama ilivyo kwenye Swala nyingine, kisha atapiga takbiri nne kama ifuatavyo:

1. Atapiga takbiri ya kwanza, nayo ni takbiri ya kufungia Swala, na ataleta Audhu.. na apige bismillahi.. na asisome dua ya kufungulia Swala, kisha asome Fatiha.
2. Atapiga takbiri ya pili, na atamswalia Mtume ﷺ kama ilivyo namna ya kumswalia Mtume katika kikao cha Atahiyatu ya mwisho.
3. Atapiga takbiri ya tatu, na atamuombea maiti. Na miongoni mwa dua ni kusema: (Ewe Mola! Mghufirie na umrehemu,

umpe afya na umsamehe, ukirimu mashukizi yake na umpanulie njia yake kuingilia (Peponi), Umsafishe kwa maji, theluji na barafu, umtakase kutokana na dhambi kama inavyo takaswa nguo nyeupe na uchafu, Umbadilishie nyumba umpe nyumba ya kheri kuliko nyumba yake alokuwa nayo, na watu wa kheri zaidi kuliko watu alokuwa nao, na mke wa kheri kuliko yule alokuwa naye, Umtie peponi na umlinde na adhabu ya kaburi, au adhabu ya Moto)[ Imepokewa na Muslim.].

Na iwapo maiti ni mwanamke kutatumika dhamiri za kike (dua isomwapo kwa Kiarabu)

Na maiti akiwa ni mtoto mdogo au ni tisha [ Siqtw: mwana wa matumboni anayezaliwa kabla ya kukamilika.] atasema: (Ewe Mola! Mjaalie ni akiba ya wazazi wake na kitangulizi chema [ Faratw: aliyetanguliwa na kuwa wa mwanzo.] na ni thawabu kwao na kiombezi mwenye kukubaliwa dua) [ Imepokewa na Bukhari.].

4. Atapiga takbiri ya nne, na atanyamaza kidogo, kisha atatowa Salamu moja upande wake wa kulia au salamu mbili.